40 HADITH

ZA WATOTO PAMOJA NA VISA

Prof. Dkt. M. Yaşar KANDEMİR

ERKAM
PUBLICATIONS

بسم الله الرحمن الرحيم

Istanbul / 2022

© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

HADITH 40 ZA WATOTO PAMOJA NA VISA

Prof. Dkt. M. Yaşar KANDEMİR

Jina la Asili: Çocuklara 40 Hadis
Mwandishi: Prof. Dkt. M. Yaşar KANDEMİR
Msimamizi Mkuu: Abdi Mohamed Adam
Mfasiri: Mohamed M. Potea
Mhariri: Ibrahimu H. Kabuga
Msanifu jalada: Sarkhan Isgandarov
Kupangiliwa vizuri na: Sarkhan Isgandarov
Nijat Garibov
ISBN: 978-9944-83-671-5
Mchapaji: Erkam Printhouse
Anuani: Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi Mah. Atatürk Bulvarı, Haseyad 1. Kısım No: 60/3-C Başakşehir, Istanbul, Turkey
Simu: (+90-212) 671-0700 pbx
(+90-212) 671-0748
Barua pepe: info@islamicpublishing.org
Tovuti: www.islamicpublishing.org
Language: Swahili / Kiswahili

ERKAM PUBLICATIONS

HADITH 40 ZA WATOTO PAMOJA NA VISA

Prof. Dkt. M. Yaşar KANDEMİR

ERKAM PUBLICATIONS

YALIYOMO

Dibaji....7
Ndege....9
Mwiba....11
Koti....13
Kioo....15
Ukatili....17
Zimwi....20
Jirani wa peponi....22
Dawa ya meno....25
Pochi....27
Sumu....29
Mkanda....31
Hasira....33
Mashindano ya kukimbia....35
Dhahabu....37
Mwizi....39
Tonge....41
Pesa....43
Mpatanishi....45
Mchezo wa kutafutana....47
Mvurugaji starehe....49

Mcheri....52
Mtoto jasiri....54
Mtoto wa mbuzi....57
Mtoto mwenye kipaji....59
Sahani ya plastiki....61
Kalamu....64
Mwongo....66
Mbuyu....69
Mwangwi....71
Mkate....73
Bakhili....75
Viatu....77
Gari....79
Moshi....81
Matofali....84
Mgeni....87
Mkata kuni....89
Tupa yenye damu....92
Mbwa....95
Ng'ombe wa manjano....97
Vyanzo vya Hadith....99

DIBAJI

Wasomaji wangu, siku zote Mwenyezi Mungu anataka waja Wake wote wawe katika furaha. Alituletea Mitume ili wafundishe jinsi ya kuwa na furaha. Mitume ni viongozi na walimu wa wanadamu. Wanatufundisha maamrisho ya Mwenyezi Mungu na namna tunavyopaswa kuishi katika huu ulimwengu. Hilo limekuwepo kuanzia kwa Mtume wa kwanza, Adamu, mpaka kwa mtume wa mwisho, Muhammad (s.a.w).

Kama mjuavyo, maneno ya Mtume wetu (s.a.w) yanaitwa *hadith*. Mtume wetu mpendwa (s.a.w), ambaye alituletea Qur'an au maamrisho ya Mola wetu, alitufafanulia maamrisho haya ya Mwenyezi Mungu kupitia hadith zake. Kupitia maneno yake alitufundisha yale tunayohitajika kuyafanya ili tuwe wenye furaha katika maisha haya na kesho Akhera.

Tunatakiwa kuyasoma mara kwa mara maneno ya Mtume wetu (s.a.w) iwapo tunataka kuyafahamu maamrisho ya Mwenyezi Mungu, na iwapo tunataka kujifunza dini yetu kwa njia kamili kabisa. Kwa karne nyingi wasomi Waislamu wameyaweka pamoja katika mashada ya hadith arobaini jambo lililowafanya wajifunze kwa urahisi.

Nami pia nilitaka kitabu changu cha hadith arobaini, ambacho nimekuandikia, kiwe mkusanyiko wa hadith arobaini za Mtume wetu Mtukufu (s.a.w). Ninajua kuwa

unapenda sana kusoma visa, hivyo nimeziwasilisha hadith hizi katika muundo wa visa vilivyoandikwa pembezoni mwa maneno ya Mtume (s.a.w). Wapendwa wasomaji wangu, ninataraji kuwa mtakisoma kitabu hiki, na iwapo mtakipenda ninawaomba mniombee dua.

Prof. Dkt. M. Yaşar KANDEMİR

NDEGE

Siku moja, mwindaji mmoja alitega mtego wake wa wavu ukingoni mwa mto. Kwa kawaida ndege wengi huwa wanavutika na punje za nafaka zinazowekwa ndani ya mtego. Ndipo huingia mtegoni. Mwindaji huyo alipokuja kukusanya nyavu zake, ghafla ndege waliruka pamoja na wavu.

Mwindaji alishitushwa na kushangazwa na ushirikiano wa ndege wale pale alipowaona wote wakiruka kwa pamoja. Aliamua kuwafuatilia ili aone nini itakuwa mwisho wao.

Njiani alikutana na mtu ambae alitaka kufahamu alipokuwa anakimbilia.

Akionesha ndege waliokuwa angani, mwindaji alisema kwamba alikuwa anaenda kuwakamata ndege.

Yule mtu alicheka na kusema: "Mungu akujaalie ufahamu! Hivi kweli unadhani unaweza kuwakamata ndege wanaoruka angani?"

Mwindaji akasema:

"Kama kungekuwa na ndege mmoja tu katika wavu nisingeweza kupata fursa hiyo, lakini subiri uone, nitawakamata wote."

Mwindaji alikuwa sahihi, kwani mara kiza kilipoingia, ndege wote walitaka kwenda viotani mwao. Baadhi yao

waliuvuta wavu kuelekea msituni, wengine kuelekea ziwani, baadhi walitaka kurukia mlimani, wengine porini. Hakuna walioshinda mwishowe wote wakaanguka na wavu hadi chini. Mwindaji akaenda na kuwakamata ndege wote.

Masikini Ndege! Kama wangejua maneno yafuatayo ya Mtume wetu (s.a.w) wangeruka katika uelekeo mmoja, na wala wasingelikamatwa na mwindaji:

"Msitengane! Kwani Mbwamwitu humla Mwanakondoo anayejitenga na kundi lake." (Nasaaii)

فَعَلَيْكُمْ بِالْجَمَاعَةِ فَإِنَّمَا
يَأْكُلُ الذِّئْبُ الْقَاصِيَةَ

رواه النسائي.

MWIBA

Hapo zamani za kale katika njia mojawapo ya mji fulani kulikuwa na adhabu za kutisha mno. Walikuwa wakiwachukuwa wahalifu na kuwaweka mbele ya simba wakali. Watu wengi walikuwa wakikusanyika ili kujionea wenyewe mandhari hayo ya kutisha.

Mhalifu zama hizo alikuwa mtumwa aliyekuwa amemkimbia mmiliki wake.

Aliwekwa katikati ya uwanja uliozungukwa na kuta ndefu pande zote. Kisha wakamleta simba mwenye njaa. Mwanzoni Simba alionekana akijiweka tayari kumvamia mtumwa yule dhalili. Lakini ghafla Simba alisitisha zoezi la kumvamia na badala yake akaanza kumrambaramba mikono yule mtumwa.

Watazamaji walishangazwa na kitendo kile, wakamuuliza yule mtumwa kwa nini Simba hakumshambulia.

Mtumwa akasema:

"Siku moja nilimuona Simba huyu msituni, akiwa amechomwa na mwiba unyayoni, na alikuwa akiugulia kwa maumivu makali, nilimtoa mwiba ule na ndipo tokea siku hiyo tumekuwa ni marafiki wazuri".

Watu wote walivutika na kisa hiki cha ajabu. Waliwaacha huru wote wawili Simba na yule mtumwa. Watu walizidi kushangazwa pale Simba alipokuwa akimfuata yule mtumwa kama paka wake.

Ajabu iliyoje ya maneno ya Mtume (s.a.w) yasemayo:

"Mwenyezi Mungu huonesha rehma zake kwa wale wenye huruma. Wahurumieni viumbe ardhini atakuhurumieni aliye mbinguni." (Tirmidhi)

الرَّاحِمُونَ يَرْحَمُهُمُ الرَّحْمَانُ، ارحموا مَنْ فِي الأَرْضِ يَرْحَمْكُمْ مَنْ فِي السَّمَاءِ

رواه الترمذي.

KOTI

Mchunga kondoo mmoja aliyejulikana kwa jina la Ahmad alikuwa ni mwenye huzuni sana. Wakati wa kipindi cha vita vikali alipoteza karibu kila alichokuwa anakimiliki. Mkewe alikufa vitani na pia alimpoteza mtoto wake wa kiume. Alipopoteza kazi yake mjini alianza kufanya kazi kama mchunga kondoo mashambani.

Siku moja wakati kondoo wake walipokuwa malishoni pembezoni mwa barabara, aliona kundi la watu wakimpeleka kijana mmoja hospitalini. Ilikuwa dhahiri kuwa kijana yule alikuwa ni masikini kuliko yeye, alikuwa akitetemeka mno kutokana na udhaifu wa jaketi lake. Kwa haraka sana, Ahmad alivua jaketi lake ambalo amelimiliki kwa miaka mingi na kumvalisha kijana yule.

Wakati yule kijana alipokuwa katika foleni ya kumuona daktari. Alishitushwa kusikia mtu akimwita yeye "baba". Alimtizama yule mtu lakini hakumfahamu. Hata yule mwitaji naye alishangazwa.

Aliomba msamaha, kwa kusema: "Samahani bwana, nimekosea, koti ulilovaa linafanana na koti la baba yangu tuliyepotezana kwa miaka mingi."

Yule mgonjwa alimuuliza kijana kuhusiana na baba yake, alikuwa nani?

Baada ya mahojiano mafupi yule mgonjwa aligundua kuwa kijana yule ni mtoto wa Ahmad Mchunga Kondoo. Alimwambia yule kijana kuwa hakuwa amekosea, na kwamba lile koti kweli ni mali ya baba yake. Baada ya kutibiwa hospitali alirudi kijijini, na kufuatana na yule kijana kisha kumuunganisha na baba yake, Ahmad mchungaji kondoo.

Ni ukweli ulioje wa maneno ya Mtume wetu Muhammad (s.a.w) yasemayo:

"Kila jema hulipwa mara kumi." (Bukhari)

إِنَّ الْحَسَنَةَ بِعَشْرِ أَمْثَالِهَا

رواه البخاري

KIOO

Hapo zamani za kale, waziri mmoja alikuwa akizunguka zunguka sambamba na maofisa wake wakubwa sokoni. Katika pitapita yake alikatisha katika soko la watumwa, ambapo watu wanaosikitisha kutokana na hali zao na kupoteza uhuru wao walikuwa wakiuzwa mmoja baada ya mwingine.

Waziri aliwasogelea watumwa wale na kutaka kuwaona kwa karibu zaidi. Mara mtumwa mmoja aliyekuwa mzee alisema kumwambia waziri:

"Kuna uchafu kwenye kilemba chako Mheshimiwa."

Waziri alivuta kilemba chake na kukikagua. Mtumwa alikuwa sahihi, hii ilimaanisha kwamba alikuwa akikatisha sokoni hali akiwa na uchafu katika kilemba chake kwa masaa yote hayo na kila mmoja aliliona hilo. Aibu gani hii! Aliwaangalia wafuasi wake kwa huzuni na kuwaambia:

"Mmeona uchafu katika kilemba changu mkaamua kufumba macho yenu na

msiniambie chochote kuhusiana na hilo. Sasa naamini kwamba rafiki yangu wa kweli ni yule mtumwa myonge. Siwezi kumuacha rafiki yangu kipenzi auzwe kama mtumwa! Mnunueni haraka na aachiwe huru."

Kisha, waziri aliandika hadith ifuatayo ya Mtume na kuituma kwa maofisa wake ili wasisahau tukio hilo:

"Muislamu ni kioo cha muislamu mwenzie."

الْمُؤْمِنُ مِرْآةُ الْمُؤْمِنِ

رواه أبو داود

UKATILI

Ilikuwa ni siku nzuri majira ya kiangazi, watoto walikuwa wakicheza michezo yao ufukweni mwa mto. Mvulana mmoja alieitwa Jafari alikuwa ni miongoni mwa watoto wanaocheza eneo hilo, Lakini watoto karibia wote walipenda kumwita "Katili" kutokana na ukatili wake kwa wanyama.

Jafari alikuwa amechoshwa na aina ya mchezo waliokuwa wakicheza, alitaka mchezo mwengine unaofurahisha na kupendeza. Wakaanza kufanya uchaguzi wa mchezo mwengine, lakini bado Jafari hakuvutiwa na machaguo yote.

Jafari akaamua kuwaita pembeni baadhi ya marafiki zake ambao walikuwa na fikra kama zake, na mara wakatangaza kuwa wamepata mchezo mzuri.

Watoto wengine walitaka kuona huo mchezo utakuwaje.

Jafari na kundi lake walimnyemelea mwenzao aliyekuwa akiitwa Ali, ambae ni mgeni wa mji na hafahamu vizuri kuogelea. Walimkamata mikono na miguu na kumtupa ndani ya mto!

Ali alipatwa na hofu kubwa, alijitahidi kuogelea, Lakini kadiri alivyozidi kuongeza bidii ndivyo alivyozidi kuzama. Alianza kupiga kelele za kuomba msaada. Jafari na rafiki zake walikuwa wakicheka alipopiga kelele.

Kwa ghafla mtoto mmoja alivua nguo zake. Alikuwa Ismail. Ismail alikuwa mtoto jasiri na ndiye pekee aliyeweze kumkabili Jafari. Mara alipoona walichomfanyia Ali aligeuka mbogo dhidi yao, Dakika chache baadae, akawa amemtoa Ali salama ufukweni.

Watoto wengine walimpongeza Ismail. Mpita njia mmoja aliyekuwa na uso wa ukarimu na mtanashati, aliona kila kilichojiri wakati ule, alimsogelea Ismail na kuweka mkono wake katika mabega ya Ismail na kusema:

“Mdogo wangu mpendwa, umefanya sawa na maelekezo ya Mtume wetu mpendwa. Allah awe radhi nawe. Mtume wetu anasema katika moja ya hadith zake:

“Muislamu ni ndugu wa muislamu mwengine.

Asimdhulumu wala kumuacha katika mikono mibaya.” (Bukhari)

الْمُسْلِمُ أَخُو الْمُسْلِمِ
لاَ يَظْلِمُهُ ولاَ يُسْلِمُهُ
رواه البخاري

ZIMWI

Hapo zamani za kale, mfanyabiashara mmoja aliekuwa akirejea nyumbani majira ya usiku akitokea katika shughuli zake, alimuona mzee, mweusi, masikini akijiandaa kulala jirani na ukuta. Hakuna mtu yeyote aliyekuwa radhi kumhifadhi mzee yule katika nyumba yake akihofia kuwatisha watoto wake. Yule mfanyabiashara akaamua kumsaidia, alimchukua hadi nyumbani kwake, akamtayarishia supu ya moto, nguo safi, na mahala pa kulala.

Usiku wa manane mzee huyo aliyekuwa amelala jirani na dirisha, aliamka na kuanza kupiga kelele. Aliwaona wezi wawili waliokuwa wakijaribu kuingia ndani ya nyumba ile kupitia dirishani.

Mzee huyo mweusi alinyoosha mikono yake na kuongea kwa sauti ya juu;

"Mnafanya nini hapo?"

"Ee Mama yangu weee! Zimwi!" Walipiga kelele wale wezi mara walipomuona mtu mweusi akiwa amevaa pajama nyeupe za kulalia, wakajirusha dirishani. Mmoja alivunjika mguu na mwengine aliumia kichwani.

Baada ya kusikia purukushani hiyo, mfanyabiashara na familia yake wote waliamka na kuwakamata wezi hao.

Ajabu iliyoje ya ukumbusho wa Mtume wetu (s.a.w):

"Mwenyezi Mungu humsaidia mja wake ikiwa mja huyo anawasaidia wenzake." (Muslim)

وَاللَّهُ في عَوْنِ العَبدِ ما كَانَ العَبْدُ
في عَونِ أَخِيهِ
رواه مسلم

JIRANI WA PEPONI

Hapo zamani za kale mfalme mmoja alikuwa akitembeatembea kuizunguka miji yake. Alibadilisha mavazi yake na kuambatana na mmoja wa watumishi wake kiasi kwamba hakuna yeyote aliyeweza kumfahamu. Alitaka kufahamu fikra za watu wake kuhusiana na utawala wake. Ilikuwa ni kipindi cha baridi na kipupwe. Aliingia katika msikiti mmoja mdogo, akawakuta watu wawili wakiwa wamekaa katika moja wapo ya kona za msikiti ule hali wakitetemeka. Hawakuwa na pahali pa kwenda. Mfalme akishangazwa na walichokuwa wakikijadili aliamua kuwakurubia.

Mmoja alikuwa akilalamika kuhusiana na hali ya hewa kuwa ya baridi; “Baada ya mauti yangu, tutakapoingia peponi, sitakubali mfalme wetu aingie peponi. Kama nitamuona akiukaribia mlango wa pepo nitavua kiatu changu na kumpiga nacho kichwani.” Mtu wa pili aliuliza, kwa udadisi;

“Kwanini umwache mfalme wetu nje ya pepo?”

“Ni hakika kabisa, sitamruhusu kuingia. Wakati sisi tunateseka hapa kwa baridi kali inayotugandisha saa hizi yeye amestarehe katika kasri lake lenye uvuguvugu. Hana habari ya hali zetu za maisha, vipi anaweza kuwa jirani yangu peponi? Sihitaji aina hiyo ya jirani huko.” Wote walicheka.

Mfalme alimwambia mtumishi wake;

“Usiusahau msikiti huu mdogo pamoja na watu hawa wawili.”

Mara mfalme aliporejea katika kasri lake, aliwatuma watumishi wake wakawalete wale wazee wawili masikini kule msikitini, pasi na kuwaeleza kilichokuwa kinaendelea.

Baada ya kusubiri kwa hofu walipelekwa katika chumba kilichokuwa kizuri na kuambiwa;

“Mtakula, kunywa na kuishi hapa na mtamuombea mfalme wetu dua kwa Mungu na msisahau kuomba awe jirani yenu peponi!”

Huruma iliyoje ya moyo wa mfalme huyu?

Mtume wetu (s.a.w) aliwasifu wale wanaosaidia wenye mahitaji katika hadith ifuatayo:

"Mwenye kusaidia mahitajio ya waumini hapa duniani, Mwenyezi Mungu ataangalia mahitajio yake huko akhera." (Muslim)

مَنْ نَفَّسَ عَنْ مُؤْمِنٍ كُرْبَةً مِنْ كُرَبِ الدُّنْيَا
نَفَّسَ اللَّهُ عَنْهُ كُرْبَةً مِنْ كُرَبِ يَوْمِ الْقِيَامَةِ

رواه مسلم

DAWA YA MENO

Siku moja jamaa mmoja mtanashati aliingia mgahawani mjini. Akamwagiza mhudumu:

"Napenda kupata nyama iliyochomwa vizuri na kachumbari, tafadhali."

Baada ya kula kipande cha kwanza cha nyama ile, alipiga ukelele kwa maumivu;

"Ahhhh! Meno yangu yanauma tena!" Jamaa mwengine aliyekuwa amebeba begi kubwa mkononi, alichukua chupa ndogo toka katika begi lake, alimkaribia, alimimina majimaji katika kipande cha pamba kilichopo mkononi mwake na kumpatia jamaa huyo mwenye maumivu na kumtaka asugue katika jino lake linalouma.

Yule mtu alifanya kama alivyoambiwa, mara akasema:

"Nashukuru bwana, sihisi maumivu tena!"

Watu wote walimsogelea yule jamaa mwenye begi na kuulizia kama wanaweza kununua ile dawa ya ajabu. Na mara moja chupa zote zilizokuwemo ndani ya begi zikawa zimekwisha.

Saa moja baadae yule mgonjwa wa meno, na yule mwenye begi walikutana stesheni ya treni, walianza kuijadili faida waliyoipata katika biashara yao pale mjini na kuji-

pongeza wenyewe. Walikaa na kuisubiri treni inayofuata. Ghafla walitokea askari wawili na kuwakamata.

Mnunuzi mmoja wa dawa ile ya bandia alienda kushitaki polisi baada ya dawa kutofanya kazi aliyoitarajia.

Mkuu wa polisi aliwaita wale watu wawili katika ofisi yake na kuwahoji:

"Ni ipi dini yenu? Nyie ni waislamu?"

Pasi na kuinua vichwa vyao walisema:

"Tunamshukuru Mungu, sisi ni waislamu"

Mkuu wa kituo alipandwa na hasira kali dhidi yao.

"Hivi hamjawahi kusikia hadith ya Mtume wetu isemayo:

"Yeyote mwenye kutufanyia ghushi (Udanganyifu) si miongoni mwetu." (Muslim).

مَنْ غَشَّنَا فَلَيْسَ مِنَّا

رواه مسلم

POCHI

Hapo zamani za kale, palikuwa na mfanyabiashara mmoja mwenye tabia mbaya ambaye alikuwa amepoteza pochi lake sokoni likiwa na sarafu mia nane za dhahabu ndani yake. Aliitafuta kila pahali, na alimuuliza kila mtu iwapo alikuwa ameoiona, lakini hakuna yeyote aliyeipata wala aliyeiona. Baadae, alimkodi mpiga mbiu ili atangaze kuwa yeyote atayeipata pochi hiyo atapatiwa zawadi nono ya sarafu mia moja za dhahabu.

Fundi viatu mmoja alieitwa Veli, aliipata pochi ile. Alikuwa ni mtu mkarimu mno. Aliamua kuihifadhi hadi ampate mmiliki wake. Mara baada ya kusikia tangazo la mpiga mbiu, alimuendea mfanyabiashara na kumrudishia pochi lake.

Mfanyabiashara hakuwa mtu wa hasira pekee; bali pia alikuwa muongo na bakhili. Alifurahi kwa kuwa pochi lake limeonekana, lakini hakulidhihirisha hilo kwa Veli.

Alilifungua pochi na kuanza kuhesabu hela akisema:

"Oh! Naona tayari umekwishachukua pesa nilizokuahidi kama zawadi."

Veli alimkunja shati na kumtikisatikisa.

"Ni mtu wa aina gani wewe! Ndio, mimi ni masikini lakini; sio mwizi au tapeli. Hutaki kunipa pesa ulizoahidi, sawa, ila usinituhumu kukuibia pesa zako!"

Baada ya mfanyabiashara kukataa kufuta usemi wake, wote wakajikuta wapo mahakamani. Baada ya kusikiliza pande zote mbili. Hakimu aligundua kuwa mfanyabiashara anaongopa, hivyo akaamua kumpatia adhabu kali.

"Mfanyabiashara anasema kuwa vipande mia moja vya dhahabu vimechukuliwa katika pochi, sawa, na fundi viatu anasema hajachukua pesa yoyote. Naziamini pande zote mbili. Nahisi pochi iliyookotwa na fundi viatu siyo ya mfanyabiashara.

Pengine ni ya mtu mwingine kabisa. Kwa hiyo, litabaki chini ya ulinzi hadi mmiliki wake halisi apatikane.

Mfanyabiashara kwa masikitiko makubwa alijutia kitendo chake, lakini alishachelewa. Hii inatukumbusha hadith ya Mtume (s.a.w) isemayo:

"Asiyewashukuru watu hatoweza kumshukuru Mungu." (Tirmidhi)

مَنْ لاَ يَشْكُرُ النَّاسَ لاَ يَشْكُرُ اللَّهُ

رواه الترمذي

SUMU

Huseni alikuwa akirejea kijijini kwao kutokea mjini. Alikuwa mwenye furaha kubwa baada ya kufanikiwa kuuza bidhaa zote alizoenda nazo sokoni mjini. Alisimama na kupumzika katika chemchem ya maji.

'Nitasinzia chini ya mti ule na kumuacha punda wangu ale kidogo." Aliwaza.

Alipokaribia kupata usingizi akakumbuka pesa zake katika mfuko wake mdogo wa pesa. Alifikiria kuziweka mahala salama zaidi. Aliufungua mfuko na kuzitazama, zote zilikuwepo na hakuna iliyoongezeka wala kupungua.

Aliziweka ndani ya shati lake na kulificha kwa kulilalia.

Bahati mbaya kulikuwa na mwizi juu ya mti, ambaye aliona kila kitu. Mwizi huyo alikuwa mtu mbaya ambaye alitumia maisha yake yote kuwadhuru wengine. Macho yalimtoka pindi alipoona mfuko wa pesa wa Huseni.

Alishuka taratibu mtini akatoa kopo la sumu na mrija. Alimimina kiasi cha sumu katika mrija.

Kimya kimya alimsogelea Huseni ambaye alikuwa amelala fofofo. Alipanga kumuua kwa kumpulizia sumu mdomoni kupitia mrija na kuchukua pesa kirahisi.

Mara mwizi alipokuwa tayari kupuliza sumu, ghafla Huseni aliamka.

Mwizi alishtuka, akaingiza sumu yote mdomoni mwake mwenyewe na kuimeza, alikufa palepale.

Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Mwenyezi Mungu humdhuru yule mwenye tabia ya kuwadhuru wenzie." (Tirmidh)

مَنْ ضَارَّ ضَارَّ اللَّه بِهِ

رواه الترمذي



MKANDA

Nihat alikuwa mtoto mtundu sana. Alipenda kuwakera ndugu zake. Alikuwa mgomvi na mfedhuli. Tabia yake ilimkera na kumhuzunisha mama yake. Siku zote alimshauri:

"Mpendwa mwanangu, Usiumize hisia za watu wengine. Usiseme maneno ya kifedhuli kwa watu."

Lakini Nihat hakukubali kuwa ana makosa. Alikuwa akisema :

"Sio makusudio yangu mama, sijafanya chochote kibaya, wananichokoza ndipo tabia yangu inakuwa hivyo."

Siku moja mama yake alimwambia ikiwa atakaa hadi jioni pasi na kugombana na yeyote basi angemnunulia mkanda aliouona ukiuzwa dukani. Nihat alikuwa akiutaka mkanda huo.

Ndugu zake waliyasikia mazungumzo yake na mama yake, hivyo wakaanza kumjaribu kwa kumchokoza na kumpinga kwa kila anachofanya. Lakini hakukasirika; Nihat aliamua kujidhibiti mwenyewe kwa mara hiyo moja.

Wakati wa jioni mama yake alimwita:

"Naona unaweza kuwa mtoto mwema kwa ajili ya mkanda. Unatakiwa kufanya hivyo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kama alivyoamrisha na sio kwa vitu rahisi kama hivi."

Lau kama mtu angemsimulia Nihat hadith ifuatayo ya Mtume (s.a.w):

"Nachukua dhamana ya kwamba mwenye kuacha ugomvi hali yakuwa amechokozwa atajengewa mji katikati ya pepo." (Tirmidh)

مَنْ تَرَكَ الْمِرَاءَ وَهُوَ مُحِقٌّ بُنِيَ لَهُ
فِي وَسَطِ الْجَنَّةِ
رواه الترمذي



HASIRA

Halit alikuwa mtoto mkakamavu mno. Angeweza kuinua stuli kwa kutumia mkono mmoja. Katika mchezo wa mieleka shuleni hakuna aliyeweza kumshinda. Mara nyingi alipendelea kupambana dhidi ya rafiki yake aitwae Nurdin.

Siku moja kama kawaida yao Nurdin na Halit walikuwa wanapambana katika uwanja wa shule. Nurdin alishindwa akakasirika sana kiasi kwamba aliamua kwenda darasani kwao na kuchorachora vitabu vyote vya Halit.

Hili lilimkasirisha sana Halit, alimrukia Nurdin na kumpiga puani.

Pua ya Nurdin ilianza kutoa damu, ikachafua nguo zake na sakafu ya darasa pia.

Wanafunzi wenzao walijisikia vibaya kuona kilichotokea. Mwalimu alimkaripia Halit na kumueleza hadith ifuatayo:

"Mtu mkakamavu sio yule mwenye uwezo wa kuwapiga wenzake wakati wa mapambano, isipokuwa mkakamavu ni yule anayedhibiti hasira zake." (Bukhari)

لَيْسَ الشَّدِيدُ بِالصُّرَعَةِ إِنَّمَا الشَّدِيدُ
الَّذِي يَمْلِكُ نَفْسَهُ عِنْدَ الْغَضَبِ

رواه البخاري

MASHINDANO YA KUKIMBIA

Husnu alikuwa mtoto mzuri sana. Bahati mbaya alipoteza uwezo wake wa kuona katika ajali ya gari, lakini hakukata tamaa katika maisha. Kila siku alionyesha kwamba anaweza kuishi pasi na kuwa tegemezi kwa wengine. Mara nyingi alikuwa anatoka kijijini kwao hadi mjini peke yake.

Kijijini kwao kuna kijana aitwae Murtaza, huyu ni kijana mwenye kiburi mno. Siku moja, Murtaza alitaka kuwepo shindano la yeye na Husnu kukimbia hadi mjini.

Husnu alikubali. "sawa lakini kwa masharti, iwapo nitashinda mbio hizo, utanipatia jaketi lako," alisema.

Murtaza alicheka, "Kama utashinda jaketi hili ni lako," alisema.

Husnu alikuwa na sharti lingine, "Nateua muda wa mashindano."

Murtaza alifikiri Husnu asingeshinda hivyo alimruhusu.

Husnu aliteua muda wa shindano hilo la mbio kuwa ni usiku usiokuwa na mwanga.

Barabara ya kuelekea mjini ilikuwa ikikatisha msituni.

Kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kuona njia hiyo haikumsumbua Husnu kama ilikuwa ni mchana au usiku. Alitembea kama alivyokuwa akifanya siku zote na kufika mjini. Lakini Murtaza alishindwa. Mara nyingi aliangukia katika mashimo na matawi ya miti yalimpiga usoni. Aliwasili mjini nusu saa baada ya Husnu.

Maskini Murtaza! Kama angeifahamu hadith ifuatayo ya Mtume wetu mpendwa (s.a.w) asingefanya hivyo:

"Allah amenifunulia mimi: Kuwa mnyenyekevu na wala usiwe na kiburi juu ya watu wengine." (Muslim)

إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ أَوْحَى إِلَيَّ أَنْ تَوَاضَعُوا
حَتَّى لَا يَفْخَرَ أَحَدٌ عَلَى أَحَدٍ

رواه مسلم

DHAHABU

Aylini alikuwa msichana mwenye kiburi na mpenda makuu. Lakini siku moja baba yake alifariki dunia na hivyo Aylin alihuzunika sana.

Siku zote alicheza peke yake katika bustani ya nyumbani kwao. Hakutaka kuweka mazoea ya mazungumzo na msichana mwenzie wa nyumba ya pili, kwa sababu msichana huyo alikuwa mwana wa masikini.

Siku moja Bedriye alikuja bustanini kwa Aylin na kusema:

"Baba yangu ni mgonjwa sana, karibu atakutwa na mauti. anataka kukuona akueleze jambo kwa ajili ya maisha yako."

Aylin alikataa kwa dharau na kusema:

"Hivi mtu masikini anaweza kuwa na kitu muhimu cha kuniambia mimi! Nyumba yenu inatoa harufu mbaya na hakuna yeyote anayependa kuingia nyumba inayonuka."

Dakika chache baadae Bedriye alirejea hali akibubujikwa na machozi machoni mwake.

"Baba yangu anataka akueleze kitu ambacho kweli ni muhimu. Baba yako kabla hajafa alikuwa na dhahabu ambazo amezizika pahala. Ni baba yangu pekee anayefahamu mahala zilipozikwa hizo dhahabu.

"Baba yako alimwambia asikueleze kuhusiana na hilo hadi utakapokuwa mkubwa, lakini kwa kuwa anaelekea

kufa anataka akuambie sasa hivi. Tafadhali fanya haraka."

Mara baada ya Aylin kusikia maneno ya Bedriye, alitoka mbio kuelekea nyumba ya jirani. Lakini alikuwa amechelewa; Yule mtu masikini alikuwa ameshakufa.

Aylin alijikasirikia mwenyewe na kuvilaumu vitendo vyake.

Je ni dhahabu pekee ndiyo aliyokuwa ameipoteza? Hapana, vilevile alipoteza nafasi ya kuingia peponi kwa sababu alionesha tabia mbaya ya kiburi kwa mtu mkubwa anayemshinda umri.

Mtume wetu (s.a.w) anasema yafuatayo kuhusu watu wa aina hiyo:

"Hatoingia peponi mtu ambaye ndani ya moyo wake mna japo mfano wa chembe ndogo ya kiburi." (Muslim)

لاَ يَدْخُلُ الْجَنَّةَ مَنْ كَانَ
فِي قَلْبِهِ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ مِنْ كِبْرٍ

رواه مسلم

MWIZI

Nuri alikuwa mkulima masikini na wa hali ya chini. Baadhi ya watu walifikiri kutokujimudu kwake kulisababishwa na kitendo chake cha kutoingilia shughuli za watu na kutokuwa muongeaji.

Siku moja, Mtu fulani asiye na busara aliiba punda wa Nuri. Nuri alikwenda sokoni kununua punda mwingine baada ya kuona kuwa punda wake ametoweka.

Alipokuwa akitembea tembea sokoni, alimuona punda wake akiuzwa. Alimuendea muuzaji na kumwambia:

"Huyu ni punda wangu nimeibiwa wiki iliyopita."

Mwizi alikuwa mtu asiye na aibu, alijibu:

"Umekosea, punda Huyu nilimnunua tangu akiwa mdogo na nimemfuga mwenyewe hadi hivi alivyo."

Baada ya Nuri kusikia maneno hayo alipata wazo. Aliyafunika macho ya punda na kusema:

"Kama huyu ni punda wako kweli, niambie ni jicho lake lipi lisiloona?"

Mwizi alisita kidogo na kisha akajibu:

"Jicho lake la kulia."

Nuri alimfunua macho na kumuonesha muuzaji kwamba jicho la kulia linaona vizuri.

"Oh! Samahani nilichanganya, bila shaka ni jicho lake la kushoto."

"Umekosea kwa mara nyingine tena." Alisema Nuri. Akimfunua jicho la kushoto. Watu wengine waliokuwa wamewazunguka pale sokoni, walikubali kuwa Nuri ndiye mwenye busara na hekima.

Mtume wetu (s.a.w) amewaelezea wote wanaoiba vitu vya wengine:

"Mwenyezi Mungu awalaani wezi" (Bukhari)

لَعَنَ اللَّهُ السَّارِقَ

رواه البخاري

TONGE

Besim alikuwa mtoto mzuri. Baba yake alikuwa tajiri, hivyo alipata karibu kila alichokitaka. Lakini hakuwa akifahamu chochote kuhusiana na maisha ya watu wenye dhiki.

Siku moja, alipokuwa akienda kucheza mpira, mbwa alianza kumfukuza. Pamoja na kujitahidi kukimbia, alikamatwa na mbwa yule katika kichochoro kimoja chembamba baada ya kujikwaa kwenye jiwe na kuanguka.

Mara baada ya kufumbua macho yake, alimuona mvulana wa rika kama lake, na mama wa mvulana huyo. Walimuokoa dhidi ya mbwa na kumchukua hadi nyumbani kwao kumsafisha jeraha lake.

Besim aliwashukuru. Alishangaa kuona samani za nyumba hiyo zilikuwa za hali ya chini na zilizochakaa mno

Wakati alipokuwa akila nao chakula cha jioni hakujisikia vizuri. Alihisi kila alipomega tonge lilimkwama katika koo lake.

Siku iliyofuata Besim alichukua chakula kilichoandaliwa na mama yake kwa ajili yake na kwenda nacho hadi kwa yule mvulana na mama yake na kula nao pamoja; safari hii, alijisikia vizuri alipokuwa anakula. Na mara wavulana hawa wawili wakawa marafiki wakubwa.

Besim alikuwa ni mtoto mkarimu na mwenye huruma, na hivyo ndivyo maisha yake yalivyolingana na hadith ifuatayo ya Mtume (s.a.w):

"Hajaniamini mimi mwenye kulala ameshiba wakati jirani yake ana njaa naye akifahamu hilo." (Ibn Abi Shaib)

مَا آمَنَ بِي مَنْ بَاتَ شَبْعَانَ وَجَارُهُ
جَائِعٌ إِلَى جَنْبِهِ وَهُوَ يَعْلَمُ بِهِ
رواه إبن أبي شيبة

PESA

Ilikuwa ni mwezi wa Ramadhani ambapo Ethem alikuwa amekwenda dukani kununua mikate kwa maandalizi ya futari. Mbele ya duka la mikate kulikuwa na foleni kubwa sana. Kadiri muda wa kufuturu ulipozidi kukaribia ndivyo foleni ilivyozidi kuongezeka.

Muuza mikate alipata hofu kutokana na wingi wa watu walio katika foleni. Haikuwa rahisi kwake kuharakisha ili kuhakikisha kila mmoja anachukua mkate na kupata pesa iliyokuwa sahihi. Ilikuwa tayari muda wa kufuturu wakati zamu ya Ethem ilipofika. Muuza mikate alikuwa amechoka kweli kweli wakati huo, kwa bahati mbaya akampa Ethem chenji nyingi. Mwanzo Ethem alisita na kumuangalia muuza mikate usoni huku akishangaa.

"Kuna kitu kimekosewa?" Muuza mikate aliuliza.

"Hapana" Ethem alisema na kuchukua pesa kisha akatoka mbio hadi nyumbani.

Wakati wa chakula cha jioni Ethem alikuwa na hofu na wasiwasi. Wasiwasi ulimuongezeka mara alipopanda kitandani usiku ule. Aliwaza kiasi cha kuhisi kuna mtu asiyeonekana akimuuliza:

"Kwanini umefanya hivyo, kwanini umechukua pesa zisizokuwa zako?"



Alifikiria kuwa amuelezee mama yake kila kitu; lakini alibadilisha fikra zake na hakusema chochote. Alifahamu kwamba mama yake atamkasirikia na kumlaumu. Usiku mzima alikumbwa na jinamizi. Alipoamka asubuhi hakujihisi vizuri, aliangalia kalenda iliyobandikwa ukutani kulikuwa na hadith ya Mtume (s.a.w) iliyosomeka hivi:

"Dhambi ni kitu chochote kinachosumbua moyo wako, na kitu ambacho hutaki wengine wakifahamu." (Muslim).

الْإِثْمُ مَا حَاكَ فِي صَدْرِكَ
وَكَرِهْتَ أَنْ يَطَّلِعَ عَلَيْهِ النَّاسُ

رواه مسلم

Ethem alihisi uso wake unakuwa mwekundu, kana kwamba Mtume wetu mpendwa (s.a.w) alisema maneno yale kwa ajili yake. Haraka sana alienda katika duka la mikate na kumpa muuza mikate pesa yake. Aliomba radhi kwa kutomrudishia mapema.

MPATANISHI

Ilikuwa majira ya baridi na kipupwe, wakati Isa alipokuwa akikimbia kuwahi shuleni, njiani akampita mtoto masikini. Mtoto huyo hakuwa amevaa hata koti. Viatu vyake vilikuwa vimechakaa na mavazi yake yamelowana. Isa alikuwa akimpita ndipo alipoona hili. Familia ya Isa haikuwa tajiri lakini walimpatia alivyovihitaji.

Isa aliamua kumfuatilia mtoto huyu. Alishangaa kuona kuwa yule mtoto anaenda shule ileile anayosoma yeye. Isa hajawahi kumuona hapo kabla. Alijiuliza kitu cha kufanya ili kumsaidia yule mtoto, angempa viatu vyake alivyovivaa lakini hakuwa na jozi ya ziada ya viatu.

Alimuona tena yule mtoto wakati wa mapumziko hivyo akaamua kumsogelea na kumuomba urafiki na mara moja wakawa marafiki wakubwa. Ndipo akagundua kuwa yule mtoto hakuwa na baba bali aliishi na mama yake pamoja na wadogo zake wa

kike wawili ambao walikuwa wamekwenda katika ujirani mwema. Walikula pamoja mchana siku hiyo.

Jioni ya siku hiyo, Isa alimwambia baba yake:

"Mwalimu ametupatia kazi leo, tunatakiwa tutafute jinsi gani tunaweza kuwasaidia masikini"

Baba yake alimpatia fikra na maelekezo ya baadhi ya njia za kuwasaidia masikini.

Siku iliyofuata Isa alienda katika taasisi inayojishughulisha na kusaidia masikini iliyokuwa jirani. Alikutana na mtu mwenye sura ya ukarimu mno, Alimuelezea hali ya rafiki yake na kumuombea msaada. Yule mtu alifurahishwa sana na kitendo cha Isa na akampongeza kwa kufanya hivyo. Alimtaka Isa aende akatafute mahala anapoishi rafiki yake kisha aje amuelezee halafu akamwambia:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake mpendwa wanawapenda watoto wenye tabia kama yako. Ulivyofanya ni kulingana na maelezo ya hadith ifuatayo:

"Hakika mwenye kuelekeza jambo la kheri atalipwa na Mswenyezi Mungu kana kwamba yeye ndiye amekifanya kitendo hicho." (Tirmidh)

إِنَّ الدَّالَّ عَلَى الْخَيْرِ كَفَاعِلِهِ

رواه الترمذي

MCHEZO WA KUTAFUTANA

Ihsan na rafiki zake walikuwa wakicheza mchezo wa kujificha na kutafutana. Ulipofika muda wa kujificha Ihsan alitafuta mahala pazuri pa kujificha nyuma ya mtaa karibu na njia. Ingekuwa vigumu kwa mtafutaji kumuona pale.

Mara mtu mmoja, mgeni, mzee mwenye mvi kichwani alimjilia pale alipokuwa amejificha.

"Kijana nahitaji maelekezo, unaweza kunisaidia?" yule mzee alisema.

Ihsan aligeuka na kuweka kidole chake mdomoni, akimuashiria yule mzee kwamba anatakiwa akae kimya.

Yule mzee hakuelewa kwanini anatakiwa anyamaze, na alimuangalia Ihsani kwa mshangao, akauliza: "Kwanini unanitaka ninyamaze?" Nakuuliza swali wewe, kama unafahamu jibu niambie basi na kama hujui nieleze. Watoto wa mjini hawaeleweki wana tabia za ajabu mno. Yule mzee alilalamika.

Mara mtafutaji alipomuona yule mzee pale nyuma ya mti akiongea na mtu alijua kwamba kuna mtu atakuwa amejificha pale. Alisogea kimya kimya.

Yule mzee, alisema kwa unyonge:

“Kwa hakika hakuna yeyote aliyewafundisha hawa watoto hadith ifuatayo ya Mtume (s.a.w):

“ Mwenye kumuelekeza aliyepotea ni sawa na mtu aliyetoa sadaka.”(Tirmidh)

مَنْ هَدَى زُقَاقًا كَانَ لَهُ مِثْلَ عِتْقِ رَقَبَةٍ

رواه الترمذي

Aligeuka na kuondoka zake. Ihsan alijisikia aibu kwa kitendo alichofanya, akasahau mchezo aliokuwa anaucheza. Alimkimbilia yule mzee na kumuomba msamaha, kisha akampeleka mahala alipotaka kufika.

MVURUGAJI STAREHE

Mara nyingi Avni alikuwa mtoto mwema, ila alikuwa na tatizo moja tu. Alikuwa mbishi mno kiasi cha rafiki zake wote kutoipenda tabia yake hiyo mbaya.

Siku moja katika majira ya kupukutika kwa majani ya miti, watoto wote walikuwa wakizungumza kuhusiana na maziwa na bahari ufukweni mwa ziwa. Walikuwa wakisema kwamba bahari ilikuwa na kina kirefu na baridi kuliko ziwa.

Kama ilivyo ada, siku zote Avni huwa na maoni yanayotofautiana na wengine. Safari hii rafiki zake hawakujadiliana nae, sasa walikuwa wakimfahamu vizuri sana.

Safari hii rafiki zake walikuwa wakirusha mawe yenye umbo la bapa na membamba kuelea usawa wa bahari ya buluu kama ndege warukao.

Faruk alikuwa na uwezo wa kurusha mawe hayo kwa umbali mrefu zaidi kushinda wengine. Avni alijisikia wivu na kusema:

"Wacha mimi nione mawe yako."

Faruk alifungua mkono wake na kumuonesha Avni. Mawe yake hayakuwa tofauti na ya wengine, lakini mvuraugaji starehe Avni hutafuta sababu ya kuzusha ugomvi.

"Oh! Umechukua mawe membamba. Bila shaka mawe membamba huenda umbali mrefu zaidi, yeyote anaweza kufanya hivyo."

Faruk hakuwa kijana mbishi alisema:

"Sawa, kwanini tusibadilishane mawe yetu! Wewe chukua yangu na mimi nichukue yako!"

Lakini matokeo yalikuwa yaleyale.

Haidari, kijana mlemavu aliyeumia katika ajali ya barabarani alimkaribia Avni. "Upo katika hali mbaya leo, na hauna bahati vilevile." Alisema kwa upole.

Avni alikasirika sababu hakuweza kurusha mawe na alimpigia kelele Haidari kwa kugomba.

“Unajua nini wewe kiwete”

Watoto wengine walimkasirikia Avni, wote walimpenda Haidar na walimchukia yeyote aliyejaribu kumfanyia ubaya, walimwambia Avni kuwa alivyofanya sio sawa na ni makosa.

Tabia ya Avni inapingana na hadith ifuatayo ya Mtume (s.a.w):

“Usibishane na ndugu yako Muislamu na wala usimdhihaki.” (Tirmidh)

لاَ تُمَارِ أَخَاكَ وَلاَ تُمَازِحْهُ

رواه الترمذي

MCHERI

Ali na Aisha waliparamia mti wa Mcheri na kuanza kula matunda yaliyoiva ya Cheri. Ali aligundua kwamba macheri yanayoning'inia nchani mwa matawi ni mazuri zaidi.

"Matawi yote ni membamba na hayawezi kuhimili uzito wako, haya ni mazuri vilevile." Aisha alimwambia Ali kumzuia asiyaendee matawi membamba.

Lakini Ali hakusikiliza. Hakuwa anawaza chochote zaidi ya macheri. Alitambaa hadi katika matawi membamba yaliyo mwisho wa mti. Kabla hajafika mbali alijikuta yu chini ya mti akiwa na tawi lililokatika. Lakini pia mguu wake uliumia, atalazimika kukaa nyumbani kwa siku kadhaa; atachofanya ni kuwatazama tu watoto wengine wakipanda mti na kuchuma macheri.

Tabia ya Ali ilikuwa ni ya ulafi mno. Haikuwa hivyo?

Onyo lililoje litokanalo na hadith ya Mtume (s.a.w) isemayo:

"Kama mwanadamu angepewa mabonde mawili ya dhahabu, bado angehitaji bonde la tatu. Kaburi pekee ndilo lenye kuweza kuuridhisha ulafi wa mwanadamu." (Tirmidh)

لَوْ كَانَ لاِبْنِ آدَمَ وَادِيَانِ مِنْ ذَهَبٍ لأَحَبَّ
أَنْ يَكُونَ لَهُ ثَالِثٌ وَلاَ يَملأُ فَاهُ إِلاَّ التُّرَابُ

رواه الترمذي.

MTOTO JASIRI

Siku nyingi zilizopita, maharamia walikuwa na kawaida ya kusubiri pembeni mwa barabara kukaba na kuwateka watu, kisha kuwauza katika soko la watumwa.

Siku moja walimteka mzee mmoja masikini, kiongozi wa maharamia alimwambia yule mzee;

"Kama hutaki sisi tukuuze katika soko la watumwa, tupatie vipande mia moja vya dhahabu; Ni hivyo tu ndipo tutakuruhusu uondoke."

Yule mzee aliamua kuandika barua kwa familia yake, akisema:

"Nafahamu kwamba hamna pesa za kutosha kununua uhuru wangu. Naandika barua hii kuwafahamisha kilichonitokea."

Mzee yule, alikuwa na mtoto mmoja mkarimu na jasiri mno. Alipopata barua ya baba yake aliwaendea maharamia na kusema:

"Enyi Mabwana! Nafahamu kwamba hamtamwachia baba yangu bila kupata malipo. Siwaombi kufanya hivyo, isipokuwa mnaona kuwa yeye ni masikini, mzee na ni dhaifu. Kama mtamuuza, hamtapata malipo makubwa. Nichukueni mimi, na mniuze badala yake, mtapata pesa nyingi zaidi kwa njia hii."

Maharamia walilipenda wazo hili, lakini wakasema kuwa wanahitaji kumuuliza kiongozi wao kwanza. Kiongozi wao hakuamini alichokisikia, alimuangalia yule mtoto jasiri kwa mshangao na kusema:

"Hivi bado dunia hii ina watoto jasiri kama wewe. Ni ajabu kiasi gani. Ningejitolea mwenyewe kuwa na mtoto jasiri kama wewe! Njoo, Kwa ujasiri wako nakupa uhai wa baba yako, wote mpo huru, mnaweza kwenda."

Mzee na mwanawe jasiri walirejea nyumbani. Walifurahi baada ya kufanikiwa kuivuka bahati mbaya iliyokuwa

ikiwakabili. Habari hii inatukumbusha hadith ifuatayo ya Mtume wetu mpendwa (s.a.w):

" Mtoto hawezi kumlipa fadhila mzazi wake ispokuwa baba yake awe mtumwa na yeye amnunue kisha amwache huru (Muslim)

لا يَجْزِي وَلَدٌ وَالِدًا إِلاَّ
أَنْ يَجِدَهُ مَمْلُوكًا فَيَشْتَرِيَهُ فَيُعْتِقَهُ

رواه مسلم

MTOTO WA MBUZI

Najib alikuwa mtoto anayependa sana mbuzi, na hasa watoto wa mbuzi. Baba yake alimpatia zawadi ya mwanambuzi mmoja mdogo. Najib alimlisha na kumkatia majani wakati wa jua. Alipenda sana mwanambuzi alipomkimbilia na kumrukia na kuipiga mikono yake kichwani.

Siku zote baba yake alimwambia Najib:

"Usiache mlango wazi, vinginevyo mwanambuzi ataingia ndani na kuharibu vitu."

Siku moja Najib alikimbilia ndani kuchukua mpira wake, alikumbuka maagizo ya baba yake, lakini hakujali kufunga mlango sababu alikuwa na haraka sana.

Hakufahamu kwamba mwanambuzi alimfuata hadi ndani.

Wakati mwanambuzi alipokuwa akimtafuta Najib, alijiona mwenyewe mbele ya kioo kikubwa kilichopo varandani. Mwanambuzi alidhani kuwa mwanambuzi mwingine alikuwemo ndani ya kioo hicho, wakati mwanambuzi alipokikaribia kioo na yule mwengine nae alifanya hivyo. Alipata wazimu alipoona mwengine anamsogelea . Mwanambuzi akainamisha kichwa, akakimbilia kwenye kioo na kukipiga kichwa, Alitaka kumpa somo yule mwanambuzi

mwingine. Kishindo kikubwa kilisikika ndani ya nyumba, Kioo kilivunjika kwa zaidi ya vipande mia moja.

Kama Najib angefahamu mafundisho ya Mtume (s.a.w) alipowaambia masahaba zake wawili wadogo, Ibn ʻUmar na Abdullah Ibn ʻAmr asingedharau usia wa baba yake:

"Mtii baba yako" (Ahmad)

أَطِعْ أَبَاكَ

رواه أحمد



MTOTO MWENYE KIPAJI

Wanawake watatu walikuwa wakirejea kutokea sokoni wakiwa na vikapu mikononi mwao. Walikaa katika benchi ili wapumzike kidogo. Walianza kujadiliana kuhusiana na watoto wao.

Mwanamke wa kwanza alianza kuelezea namna mtoto wake alivyokuwa hodari kiasi kwamba anaweza kutembea kwa dakika kadhaa akiwa anatumia mikono.

Wa pili akasema mtoto wake anaweza kuimba vizuri sana na kila mmoja akavutiwa na uimbaji wake.

Mwanamke wa tatu alisikiliza tu, mwenzake akamuuliza kwa nini yeye hasemi chochote. "Mtoto wangu hana kipaji maalumu ninachoweza kumsifia." Alisema.

Mzee mmoja aliekuwa akipita karibu yao alisikia majadiliano yao na kuamua kuwafuatilia. Wakati akinamama hao walipoingia katika mtaa wanaoishi walisimama tena kupumzika, wakaweka vikapu vyao chini, na mara watoto wao wakawaona na kuanza kuwakimbilia.

Mtoto wa yule mama wa kwanza alikuja akiviringika kisarakasi.

Mtoto wa yule mama wa pili alikuja akiimba moja ya nyimbo zinazopendwa na mama yake. Wanawake wote walimpigia makofi.

Mtoto wa yule mama wa tatu alikuja na kuuliza:

"Naweza kukusaidia mama?" na akachukua kikapu.

Wanawake wale walimsimamisha yule mzee na kumuuliza anafikiri ni mtoto yupi mwenye kipaji.

"Nimeona mtoto mmoja tu ndie mwenye kipaji." Alisema: "Ni yule aliyekimbilia na kumsaidia mama yake kuchukua kikapu. Ameonesha mwenendo kulingana na hadith ifuatayo ya Mtume (s.a.w):

"Namuusia kila mtu kumhudumia na kumtumikia mama yake." (Ibn Majah)

أُوصِي امْرَأً بِأُمِّهِ

رواه ابن ماجه

SAHANI YA PLASTIKI

Kulikuwa na fundi seremala mmoja, masikini na mzee. Nguvu zake zilishapotea na tayari alikuwa ameanza kupoteza nuru ya macho yake. Kwa sababu ya kutetemeka kwa mikono yake hawezi kushika kijiko cha chakula vizuri. Chakula kilichomwagikia katika kitambaa cha meza ni kingi kuliko alichobahatika kukiingiza mdomoni mwake.

Mwanae na mkwewe siku zote walimtaka awe mwangalifu. Walimkasirikia sana, hasa wakati chakula kilipodondoka chini ya kidevu. Hatimae walimuweka katika meza ya peke yake mbali na wao.

Mjukuu wake mdogo aliyeitwa Hasani alihuzunishwa sana na hali ya babu yake hivyo kuamua kumsadia kwa kumshikia kijiko ili asimwage chakula.

Siku moja, kwa bahati mbaya, wakati akila yule mzee alianguka na kuvunja sahani. Aliwatazama wanawe waliokaa mezani, machozi yakimlengalenga.

Walikasirika sana, walimkaripia na kumvunja moyo. Kuanzia siku hiyo walimtengea chakula chake katika sahani ya plastiki.

Siku moja, mtoto wa fundi seremala alimwambia mkewe asiweke matunda katika sahani ya baba yake na aichukue sahani hiyo ya plastiki na kuitupa katika pipa la takataka.

Hasani aliichukua sahani na kumwambia mama yake asiitupe mbali sababu wataihitaji katika siku za baadae.

"Unaitaka ya nini?" Baba yake alihoji.

Hasani akajibu:

"Nitaitumia kwa ajili ya chakula chenu mtapokuwa wazee kama babu."

Wazazi wa Hasani walijisikia aibu, walinza kula tena pamoja na baba yao.

Kama yule mtoto na mkewe wangefahamu kwamba njia bora ya kuwapeleka peponi ni kuwajali wazazi wawili, kwa hakika wasingefanya hivyo:



Mtume wetu mpendwa (s.a.w) analielezea suala hili katika hadith ifuatayo:

"Radhi za Allah zipo pamoja na radhi za wazee wawili na hasira za Allah zipo pamoja na hasira za wazee wawili." (Tirmidh)

رِضَى الرَّبِّ فِي رِضَى الْوَالِدِ
وَسَخَطُ الرَّبِّ فِي سَخَطِ الْوَالِدِ
رواه الترمذي

KALAMU

Jalal alikuwa mtoto wa fundi seremala masikini. Alikuwa amekaa kwenye kona ya mtaa akilia kwa sababu alikuwa amepoteza kalamu yake.

Mtu mmoja aliyekuwa amevaa vizuri alikuwa akipita njia. Alisimama na kumuuliza Jalal kilichokuwa kikimliza. Alipolisikia tatizo lake alichukua kalamu mfukoni mwake na kumuuliza:

“Je hii ndiyo kalamu uliyoipoteza?”

Jalal akajitahidi kunyamaza na kujibu:

“Hapana, hii siyo. Kalamu yangu haikuwa nzuri kama hiyo”.

Mtu huyo alistaajabu kwa uaminifu wa Jalal.

“Kwa kuwa wewe ni kijana mwaminifu na unasema ukweli, ninakupatia kalamu hii kama zawadi. Tafadhali ipokee”.

Katika hadith ifuatayo Mtume wetu (s.a.w) ametueleza jinsi Mwenyezi Mungu atakavyowalipa watu wakweli:

“Hakika kusema ukweli kunampeleka mtu kwenye wema na wema humpeleka peponi” (Bukhari).

إِنَّ الصِّدْقَ يَهْدِي إِلَى الْبِرِّ
وَإِنَّ الْبِرَّ يَهْدِي إِلَى الْجَنَّةِ

رواه البخاري

MWONGO

Siku moja mwanaume na mwanamke walikuwa na kesi mahakamani. Mara baada ya hakimu kuingia baraza likaanza na mwanamke akatakiwa kutangulia kutoa maelezo.

Akimuashiria mkono wake kuelekea kwa mwanaume mwembamba aliyesimama jirani naye, alisema:

"Huyu jamaa alinishambulia na kunipora heshima yangu." Akaanza kuomboleza.

Yule mwanaume akajitetea mwenyewe kwa kusema:

"Anaongopa mheshimiwa. Nilipokuwa nikihesabu pesa nilizozipata baada ya mauzo yangu ya kondoo, huyu mwanamke alinifuata akinitaka nimpatie hizo pesa, alinitisha akisema kwamba kama sikumpatia hizo pesa atanisababishia matatizo. Nilipokataa alianza kupiga kelele."

Baada ya kuwasikiliza hakimu alifahamu ni yupi miongoni mwao mkweli na yupi anaongopa. Lakini hakusema kitu.

Akamgeukia yule mwanaume na kumwambia kwa hasira:

"Umemshambulia huyu mwanamke dhaifu, halafu unakuja kutueleza mlima wa uongo hapa, mpe pesa zote zilizo mfukoni mwako huyu mwanamke vinginevyo nitakuweka jela."

Kila mmoja mahakamani alishangazwa, kwa kuwa hawakutarajia hakimu awe katika hali ile.

Mwanamke kwa furaha alichukua pesa za yule mwanaume na kuondoka katika chumba cha mahakama huku akimuombea dua hakimu. Mara alipotoka, Hakimu alimwambia yule mwanaume amfuate yule mwanamke akachukue pesa zake.

Yule mwanaume alishangaa kwa mara nyingine na bila kuchelewa alitoka nje kwenda kuchukua pesa zake.

Dakika chache baadae, walirejeshwa tena mahakamani, mwanaume akiwa amevilia damu na ana michubuko usoni.

Kwa mara nyingine Mwanamke alikuwa wa kwanza kuzungumza. Alikwa na hasira.

"Mheshimiwa, huyu mfidhuli aliamua kuja kuchukua tena pesa ulizonipa."

Hakimu alimuuliza yule mwanamke:

"Aliweza kuchukua hizo pesa?"

"Hivi unadhani naweza kumpatia chochote huyu mwanaume." Yule mwanamke alijibu kwa dharau.

Hakimu aligeuka na kumkaripia yule mwanamke:

"Wewe ni muongo, tena usie na haya! Unajifanya kama mwanamke mwema, ukimshutumu huyu mwanaume kukushambulia, kama hilo lingekuwa sahihi ungepambana kwa bidii kujiokoa mwenyewe kuliko kuokoa pesa zisizo kuwa zako. Sasa hivi mpe pesa zake haraka."

Kabla hajampa adhabu, Hakimu alimkumbusha yule mwanamke hadith ifuatayo ya Mtume wetu (s.a.w):

"Jihadhrini na uwongo, hakika ya uongo huongoza katika uovu, na uovu huongozo motoni." (Muslim)

إِيَّاكُمْ وَ الْكَذِبَ فَإِنَّ الْكَذِبَ يَهْدِي إِلَي
الْفُجُورِ وَ إِنَّ الْفُجُورَ يَهْدِي إِلَي النَّارِ

رواه مسلم

MBUYU

Husnu alikuwa akimwambia hakimu, akimuashiria mtuhumiwa:

"Mheshimiwa! Nilimuachia huyu jamaa pete ya almasi kabla sijasafiri nje ya nchi mwaka uliopita, sasa hivi naitaka pete yangu lakini yeye hataki kunipa."

Hakimu alimuuliza Mistik Kahaya, ambae alikuwa amekaa katika kizimba.

"Kwanini hujamrudishia pete yake?"

"Anadanganya, hakunipatia pete." Mistik Kahaya alijibu.

Hakimu alimgeukia Husnu:

"Unae shahidi aliyeona ukimpatia huyu bwana hiyo pete?"

“Hapana, hakukuwa na yeyote pamoja nasi wakati nampa tulikuwa chini ya Mbuyu.”

Hakimu alimtaka Husnu aende akalete tawi la Mbuyu.

Dakika chache baadae, hakimu alimgeukia Mistik Kahaya na kumwambia:

“Atakuwa wapi? Sijui atarudi muda gani, Nenda dirishani umwngalie na ukimuona anarudi uniambie.”

Pasi na kusogea wala kushtuka, Mistik Kahaya alijibu:

“hawezi kurudi chini ya masaa matatu. Ni mbali kutoka eneo hili.”

Hakimu alimgeukia Mistik Kahaya na kusema:

“Wewe si muongo peke yeke bali pia ni mpumbavu. Kama hukuchukua pete usingefahamu mahali ulipo huo mbuyu, Hivi hujapata kusikia hadthi ya Mtume wetu?

“Enyi watu! Jihadharini na uongo, kwani uongo na imani haviwezi kuwa pamoja.” (Ahmad)

يَا أَيُّهَا النَّاس إِيَّاكُمْ وَ الْكَذِبَ فَإِنَّ الْكَذِبَ
مُجَانِبٌ لِلإِيمَانِ
رواه أحمد

Hakimu alimpa adhabu kali kwa uhalifu wake.

MWANGWI

Mtoto mmoja aitwae Remzi alikuwa akimpelekea chakula baba yake aliyekuwa akifanya kazi shambani. Aliona kitu chenye umbile la kivuli nyuma ya mwamba juu ya kilima.

Akidhani kuna mtoto mwingine alimpigia kelele akisema "Heeey!", Sauti ilirudi na kusema: "Heeey!" kutokea katika kilele cha mlima.

Pasi na kufahamu kuwa ilikuwa ni mwangwi, alidhani kuwa mtoto mwengine alikuwa kule juu, akimfanyia mzaha.

"Hebu subiri uone kitachotokea nitapokuja huko juu"

Sauti ilijibu:

"Hebu subiri uone kitachotokea nitapokuja huko juu"

Remzi akapandwa na hasira na kupiga kelele kwa sauti ya juu:

"Jitokeze, tuonane, wewe ni mwoga!"

Mara alipopata tena jibu lenye kujirudia, alianza kukimbia kuelekea mlimani. Hadi anachoka alikuwa bado hajamuona huyo mtoto mwengine. Alifikiria kuwa yule mtoto alijificha pahala, alipanda miamba akiita kila upande, alifikiria kitu atachofanya baada ya kumtia mikononi huyo mtoto. Lakini mtoto yule mwoga hakujitokeza.

Baada ya muda mrefu, alimkumbuka baba yake. Lazima atakuwa na njaa kali mno sasa hivi. Alipofika kwa baba yake, alimsimulia kila kitu kilichotokea njiani. Baba yake alimsikiliza mwanawe na kumkumbusha usemi ufuatao:

"Yeyote anayeongea kila anachojisikia basi husikia hata asichohitaji kusikia."

Kama Remzi angeyafahamu maneno yafuatayo ya Mtume wetu asingefanya hivyo:

"Mtu mwenye kumuamini M/mumngu na siku ya mwisho basi azungumze ya kheri au anyamaze." (Bukhari)

مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ
وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَلْيَقُلْ خَيْرًا أَوْ لِيَصْمُتْ
رواه البخاري

MKATE

Ilikuwa siku yenye ubaridi na kipupwe. Hasani alikuwa akirejea nyumbani kutokea dukani alikoenda kununua mikate. Mbwa mwembamba na dhaifu sana, aliifuata mikate iliyo katika kikapu cha Hasani na kulialia akiashiria kuhitajia mikate.

Hasani alipokuwa karibu zaidi na mbwa yule mnyonge alimwangalia kwa masikitiko makubwa. Alijiambia mwenyewe "Kama nitampa moja ya mikate hii, huyu mbwa mnyonge, mama yangu atakasirika sana." Mwishowe akaamua kwamba ni bora kupata lawama za mama yake. Aliweka kikapu chake chini akachukua mkate mmoja na kumkatia yule mbwa.

Mtu mmoja aliyekuwa akija nyuma yake kutokea duka la mikate vile vile aliyasikia maneno ya Hasani. Kwa siri akamuwekea mkate mwingine katika kapu la Hasani.

Wakati Hasani alipowasili nyumbani alishangaa kuona ana mikate zaidi ya aliyoinunua dukani!

Bila shaka Hasani angelieleza hili kama angeifahamu hadith ifuatayo ya Mtume (s.a.w):

“Sadaka haipunguzi mali.” (Muslim)

مَا نَقَصَتْ صَدَقَةٌ مِنْ مَالٍ

رواه مسلم

BAKHILI

Mjomba wake Ihsani alikuwa mtu bakhili sana. Alikonda kwa sababu ya ubakhili wake. Hakuwa anapenda kutumia hela yake kwa matumizi yake binafsi wala kumpa mwingine. Hakuna aliyempenda kutokana na tabia yake hii.

Masikini bakhili huyu siku moja alibadilisha kila anachokimiliki kwa dhahabu, kwa sababu alikuwa na tamaa ya kuona kuwa kabla ya kifo chake anamiliki kila kitu. Halafu akazifukia dhahabu zote bustanini kwake.

Kila siku anazifukua na kuzihisabu moja baada ya nyingine; kisha anazifukia tena sehemu ileile.

Siku moja alipofukua hakuziona dhahabu zake, lazima kuna mtu atakuwa ameziiba. Alichanganyikiwa na kupandwa na hasira kali.

Ihsan alifahamu kilichotokea, alienda kumtembelea mjomba wake na kumwambia:

"Huna haja ya kulia kwa ajili ya pesa, hazikuwa zako. Kama zingekuwa zako usingelizizika bustanini, bali ungezitumia kwa manufaa yako."

Mtume wetu (s.a.w) ambaye alijiepusha na ubakhili kwa kukimbilia kwa Allah, alisema katika hadith yake:

"Mtu bakhili yupo mbali na Mwnyezi Mungu, mbali na pepo,na yuko mbali na watu." (Tirmidh)

الْبَخِيلُ بَعِيدٌ مِنْ اللَّهِ بَعِيدٌ

مِنْ الْجَنَّةِ بَعِيدٌ مِنْ النَّاسِ

رواه الترمذي

VIATU

Ilikuwa kipindi cha baridi kali, Sadi alihisi baridi kali sana, kwa kuwa viatu alivyokuwa amevivaa vilikuwa vimeingia maji. Kwa mara ya kwanza, alisikitika kuona kuwa familia yake ni masikini. Alifikiria aina ya uzuri wa maisha wangekuwa nayo kama wangekuwa na pesa ya kutosha kununua koti na viatu vizuri.

Siku moja, Sadi akiwa na begi lake mkononi akirejea kutoka shuleni, alisimama karibu na msikiti kwa kuheshimu adhana iliyokuwa ikiadhiniwa. Sadi anapenda kuswali msikitini, hivyo alikwenda sehemu ya kutawadhia,

aliacha begi lake la shule katika benchi na kukunja mikono ya shati lake.

Alifahamiana karibu na kila aliekuwa akitawadha pale.

Alikaa katika bomba na kuanza kuvua viatu vyake, soksi zake zilikuwa zimelowa na zimechoka mno. Kwa hasira alirusha moja ya viatu vyake chini, mara akamuona mtu aliyekuwa akitawadha jirani nae, aliosha mguu wake mmoja kisha akasimama.

Sadi akatambua kuwa yule jamaa anao mguu mmoja tu.

Hapo akatahayari, alihofia viatu vyake, lakini yule mwenzake anao mguu mmoja tu, huenda anazo pesa nyingi za kununua viatu lakini hana mguu wa kuvalia viatu hivyo. Hivyo pesa si kila kitu.

Baada ya kumaliza swala yake, Sadi alianza kumuomba Mwenyezi Mumgu na kumshukuru kwa kupata miguu mizuri.

Uzuri ulioje wa maneno ya Mtume wetu mpendwa:

"Kuwa mwenye kutosheka, utakuwa mtu mwenye kushukuru." (Ibn Majah)

وَكُنْ قَنِعًا تَكُنْ أَشْكَرَ النَّاسِ

رواه ابن ماجه

GARI

Hikmet alikuwa mwanafunzi mzuri sana. Alikuwa anakwenda shule ya sekondari (upili) mbali na nyumbani kwao. Kila siku alienda shule kwa basi na kurudi nyumbani kwa basi.

Hikmet alikuwa anapenda vitu vingi sana, miongoni mwa vitu hivyo ilikuwa ni gari. Njiani alipokuwa akielekea shuleni, alikuwa akiwaeleza rafiki zake muundo na aina ya kila gari alilopishana nalo. Alikuwa mwenye huzuni kiasi kwa kuwa familia yao haikuwa na gari. Lakini, hakuwahi kulalamika juu ya hilo katika familia yake, kwa sababu alijua kwamba hawakuweza kununua gari. Baba yake alikuwa ni mtumishi wa umma na alikuwa akipata mshahara unaotosha kulisha familia yao ya watu wanne. Itakuwa ajabu kutaka gari. Haitakuwa vizuri kutaka mengi zaidi kutoka kwa baba yake.

Rafiki yake Hikmet aitwae Ahmad alikuwa akiishi nae jirani. Yeye alikuwa hapandi basi kwenda shule. Alikuwa akitembea kwa miguu siku zote kwenda na kurudi shule. Hikmet hakuwahi kufahamu kwanini rafiki yake alifanya hivyo.

Siku moja ilikuwa baridi na mvua inanyesha. Hikmet alikuwa akisubiri na rafiki zake kituoni. Walimuona Ahmad akikatisha mbele yao akiipuuza mvua.

“Ahmad! Basi linakuja sasa hivi, kwanini unatembea?” hikmet aliuliza.

“Ahsante! Kuna pahala napitia mara moja,” Alijibu huku akiendelea kutembea.

Tukio kama hilo lilizidi kujitokeza tena kwa mara nyingine zaidi. Hikmet alianza kushangaa kwanini Ahmed hakuwa anapanda basi. Siku moja alimueleza mama yake jambo hilo.

Mama yake Hikmet aliifahamu familia ya kina Ahmed vizuri sana. Baba yake Ahmed alifariki miaka mingi iliyopita, akiacha watoto sita. Mama yake masikini alijaribu kupata pesa za kuilisha familia yake kwa kusafisha nyumba za watu wengine. Ahmed hakuweza kupanda basi kwa sababu familia yake haiwezi kumudu gharama za kupanda basi.

Hikmet alijisikia vibaya na kuona aibu. Alitamani kuwa na gari wakati kuna maelfu ya watu hawana hata pesa ya kula au hawana nyumba nzuri ya kulala. Alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila kitu alichokuwa nacho.

Kama Hikmet angeisikia hadith ifuatayo ya Mtume wetu (s.a.w) asingejisikia vibaya kwa kutokuwa na gari:

“Angalieni wale waliokuwa chini yenu na wala msiwaangalie waliokuwa juu yenu kiuwezo.” (Muslim)

انْظُرُوا إِلَى مَنْ أَسْفَلَ مِنْكُمْ
وَلاَ تَنْظُرُوا إِلَى مَنْ هُوَ فَوْقَكُمْ

رواه مسلم

MOSHI

Hapo zamani za kale kulikuwa na mtu aliekuwa akiitwa Hatem. Alikuwa ni tajiri na mkarimu mno. Alikuwa na makundi mengi ya wanyama ambao walikuwa wanakula katika eneo lenye majani, na alipenda kuchangia mali yake na wengine.

Hatem alikuwa na Farasi mweusi aliemwita Moshi. Kila mmoja alimpenda Farasi huyu kwa kasi yake. Alikuwa akikimbia kama Tai anayeruka. Hatem alimtizama Moshi kama mboni ya jicho lake na hakumkatisha tamaa kwa chochote.

Hatimaye, habari za uwezo wa mali wa Hatem na Farasi wake mzuri zilifika kwa Mfalme.

Mara mfalme aliposikia hilo alimwita waziri wake mkuu na kumwambia:

"Nataka kuujaribu ukarimu wa Hatem. Mwambie anipatie Moshi wake. Tuone nini atafanya."

Watu wa mfalme walianza safari siku iliyofuata. Usiku mmoja wenye mvua waliwasili kwa Hatem na kuwa wageni wake.

Hatem aliwakaribisha kwa furaha na bashasha. Aliwaagiza watumishi wake waandae chakula kwa ajili ya wageni

wake. Mara meza nzuri iliandaliwa kwa ajili ya chakula na wote waliizunguka kwa ajili ya kula. Baada ya chakula, wageni waliandaliwa vitanda vizuri, na walilala kwa utulivu kabisa.

Siku iliyofuata baada ya wageni kuelezea kilichowaleta, Hatem alijisikia huzuni sana na hakufahamu nini afanye kwa majonzi yale.

”Ninasikitika!” alisema, “Nilitaraji mngenieleza Mfalme alichokuwa anakihitaji tangu siku mlipowasili. Najua kwamba mnapenda nyama ya Farasi, na usiku uliopita, kutokana na hali ya hewa sikuweza kuwatafutia chochote kingine cha kula, hivyo nilimchinja Moshi na sikuwa na njia nyingine.”



Lakini ukarimu wa Hatem hauwezi kulinganishwa hata kidogo na ukarimu wa Mtume ambae alimpatia mtu mmoja ngamia mia moja!

Mtume wetu mpendwa (s.a.w) amesema katika hadith ifuatayo kuhusu wale wenye tabia ya ukarimu kuwa:

"Mtu mkarimu yupo karibu na Allah, karibu na pepo, karibu na watu, mbali na moto." (Tirmidh)

السَّخِيُّ قَرِيبٌ مِنْ اللَّهِ قَرِيبٌ مِنْ الْجَنَّةِ قَرِيبٌ
مِنْ النَّاسِ بَعِيدٌ مِنْ النَّارِ
رواه الترمذي

MATOFALI

Hapo zamani za kale alitokea mtu mmoja masikini aliejulikana kama 'Murat Mwaminifu." Alikuwa ni mtu mwenye moyo mzuri na Muislam wa dhati. Siku moja aliokota kipande cha dhahabu kilichokua katika umbile la tofali lililokaushwa kwa jua wakati alipokuwa akitengeza ukuta wa nyumba yake. Alifurahi kiasi cha kutokufahamu nini afanye.

Alianza kuwaza: "Hatimaye sio masikini tena. Nitajenga kasri kwa ajili yangu na kupamba vyumba vyake kwa samani nzuri na kuremba sakafu kwa jasi. Bustani itajaa maua na aina zote za matunda ambapo ndege wazuri watakuwa wanaimba.

Usiku ule alikuwa na ndoto nzuri sana.

Siku iliyofuata, alianza kuvuta taswira ni watumishi wangapi atakuwa nao, watunza bustani, wapishi, na watumishi wakuu ambao wote watafanya kazi katika kasri lake.

Siku iliyofuata aliendelea kuota vitu vizuri vizuri. Usiku na mchana aliota tu; Hakupata hata nafasi ya kula, kunywa, wala kumuomba Mungu na kumshukuru kwa afya njema, na ukwasi aliopewa!

Siku moja alipokuwa akitembea nje ya mji, akiota ndoto zake, alimuona mtu akitengeneza matofali kwenye

ukuta wa makaburi. Jamaa alikuwa anachimba udongo na kuuchanganya na maji na majani makavu kisha anauweka katika kielezo kutengeneza tofali.

Yule jamaa alimwambia Murat kuwa matofali yalioyotengenezwa kwa kutumia udongo wa makaburini ni imara kuliko yanayotengenezwa kwa udongo mwingine. Murat alishtuka, alihisi kana kwamba amekosea,

Ghafla aliamka kutoka katika ndoto zake na kuendelea akijikemea mwenyewe.

“Aibu iwe kwako ewe masikini usie na fikra sawa! Siku moja watatengeneza matofali katika udongo unaokufunika wewe. Umepoteza njia yako ulipokuwa unawaza hiyo dhahabu, ulimsahau Mungu wako, ukaacha kuswali na kumshukuru Mungu. Unakaribia kifo kila siku inayopita. Acha kuota na jiandae kwa mauti yako! Hii ni zawadi toka kwa Mungu; Tumia pesa zako kwa busara, usizipoteze na wala usitumie kwa mambo potofu!”

Ni hapo tu, adhana kwa ajili ya swala ya adhuhuri iliposikika.

Aliposikia hilo, Murat alienda moja kwa moja msikitini, akiwa na amani moyoni mwake; Sasa alifahamu lipi ni sahihi na zuri.

Kama Murat angeifahamu mapema hadith ifuatayo ya Mtume, asingepatwa na muda wote huo wa kuchanganyikiwa:

“Kama ningalikuwa na dhahabu mfano wa mlima wa Uahud, nisangalitaka kuiweka karibu yangu japo kwa siku tatu tu, zaidi ya ile niliyokuwa nayo kwa ajili ya madeni yangu tu.” (Bukhari)

لَوْ كَانَ لِي مِثْلُ أُحُدٍ ذَهَبًا مَا يَسُرُّنِي
أَنْ لاَ يَمُرَّ عَلَيَّ ثَلاَثٌ وَعِنْدِي
مِنْهُ شَيْءٌ إِلاَّ شَيْءٌ أُرْصِدُهُ لِدَيْنٍ
رواه البخاري.

MGENI

Hamdi alikuwa akicheza bustanini alipomuona mtu masikini mwenye nywele nyeupe akikatisha mtaani. Yule mtu alikuwa akitembea taratibu mno. Alisimama getini kwa akina Hamdi, jengo zuri sana, kupumzika.

"Mwanangu, utajali kama nitalala usiku huu katika nyumba hii ya wageni?" Alisema.

"Hii siyo nyumba ya wageni." Hamdi alimjibu, hali akitabasamu.

"Ni nini sasa?"

"Ni nyumbani kwetu."

"Kweli? Ni vizuri, Sawa… Nani amelijenga kasri hili?"

"Babu yangu"

"Nani ameirithi baada yake?"

"Baba yangu"

"Hivyo, nani atairithi baada ya baba yako?"

"Ni hakika mimi tu"

Yule mzee alitabasamu na akamuangalia Hamdi usoni kwa muda kidogo kisha akasema:

“Kama mmiliki wa nyumba hii anabadilika, hivyo inamaanisha nyinyi nyote ni wageni katika nyumba hii, Sivyo? Kisha alisimama na kuendelea kutembea.

Wakati shule ilipofunguliwa mwaka ule, Hamdi alisimulia kisa hiki katika kipindi chao cha dini. Wakati baadhi ya wanafunzi walipodhani kuwa yule mzee aliongea takataka, Mwalimu wao aliwakumbusha hadith ifuatayo ya Mtume wetu (s.a.w):

”Sikuwa mimi katika dunia ispokuwa ni kama msafiri anayeendelea na safari yake baada ya kupumzika chini ya mtu.” (Tirmidh)

مَا أَنَا فِي الدُّنْيَا إِلاَّ كَرَاكِبٍ اسْتَظَلَّ
تَحْتَ شَجَرَةٍ ثُمَّ رَاحَ وَتَرَكَهَا
رواه الترمذي

MKATA KUNI

Katika zama za Nabii Musa (a.s) alikuwepo mkata kuni mmoja. Alikuwa akikusanya kuni kutoka milimani, akizibeba mgongoni mwake, na kuziuza sokoni. Aliishi kwa kutegemea kipato kidogo alichokipata kwa kazi hiyo. Kazi ilikuwa ngumu sana, lakini mkata kuni hakuchoka.

Jirani yake mmoja alikuwa akifanya kazi hiyo hiyo, lakini alikuwa na punda wa kubebea kuni hadi sokoni. Hili lilimtia wivu sana mkata kuni.

Siku moja mkata kuni masikini alienda kwa Musa (a.s) kumuelezea tatizo lake.

"Siku zote ninakuwa na majeraha mengi mgongoni mwangu kutokana na kubeba kuni. Sijaishi kwa amani siku nzima. Tafadhali, utakapokuwa mbele ya Mola muelezee hali yangu na mwambie anipatie Punda nibebee kuni kuzipeleka sokoni.

Pindi Musa alipomuomba Mungu jambo hilo, alirudia yale aliyoelezwa na mkata kuni.

Allah alimjibu:

"Huyo ni mja wangu anaesumbuliwa na wivu, Hatofarijika mpaka aondokane na maradhi haya. Ni lazima aachane nayo. Kipindi hiki yule punda wa jirani yake anaumwa. Mwambie amuombee punda wa jirani yake. Kama atafanya hivyo na punda wa rafiki yake akawa mzima nitampatia punda."

Musa (a.s) alipomfikishia hilo mkata kuni, alijisika wivu zaidi akasema:

"Hapana, siwezi kumuomba Mungu kwa ajili ya nafuu ya punda wa jirani yangu, najisikia furaha kwa jinsi nilivyo na wala sitaki punda kutoka kwa Mungu tena. Natumai hatamtibu punda, hiyo itakuwa inatosha kwangu mimi."

Wivu ni ugonjwa. Kama mtu anaumwa ugonjwa huo, siku zote hawezi kuwa na furaha. Hiyo ndiyo sababu mkata kuni hajawawahi kujisikia furaha katika maisha yake.

Ni wa ajabu kiasi gani Mtume wetu mpendwa alipoelezea hali hii katika hadith ifuatayo!

"Jihadharini na uhasidi, kwani hakika ya husda inakula mambo mema kama moto unavyokula kuni." (Abu Daud)

إِيَّاكُمْ وَالْحَسَدَ فَإِنَّ الْحَسَدَ يَأْكُلُ الْحَسَنَاتِ
كَمَا تَأْكُلُ النَّارُ الْحَطَبَ

رواه أبو داود

TUPA YENYE DAMU

Siku moja Adam alikuwa anakwenda kununua vitu. Aliamka mapema sana asubuhi na kuelekea sokoni. Aliweka kitu kimoja baada ya kingine alichonunua sokoni katika mkoba wake wa bidhaa. Hakufahamu kwamba tupa aliyoinunua ilichana mfuko wa maini aliyoyanunua buchani.

Wakati Adam aliporudi nyumbani toka sokoni, alichukua tupa yenye damu na kuiacha mlangoni ili aisafishe. Dakika chache baadae alihisi kuwa paka mwenye njaa alivutiwa na harufu ya maini na alikuwa akiiramba tupa kwa ulimi wake.

Kitu cha ajabu ni kwamba damu katika tupa ilikuwa ikiongezeka badala ya kupungua.

Adam alijisikia vibaya, akamfukuza paka ili kumlinda.

Paka alienda pembeni kidogo na kumlilia Adam, alikuwa na njaa na alihitaji chakula, na kwanini mtu huyu alimfukuza.

Kitu ambacho paka hakukielewa ni kuwa damu aliyokuwa akiila ilikuwa ni yake mwenyewe. Alijikata ulimi wake kwa ncha za tupa. Adam alipomwambia baba yake kilichotokea alicheka na kusema:

"Baadhi ya watu ni kama paka wako, hawaamini kwamba makosa wanayoyafanya yanaweza kuwadhuru wenyewe siku moja. Wanakuwa wakali wakati watu wanapowaeleza, kama alivyo huyo paka."

Adam alilalamika: "Tunatakiwa kuwaacha wafanye makosa ili wajifunze kupitia makosa yao wenyewe."

Baba yake alimsikia na kumjibu:

“Kuwaacha na makosa yao ni makosa vilevile kwa upande wetu, tunatakiwa tujaribu kwa kadri ya uwezo wetu kuwazuia kufanya makosa, kwa njia hiyo hatuwasaidii hao watu pekee, bali jamii kwa ujumla.”

Kisha alimsomea Adamu hadith ifuatayo:

“Mwenye kuona miongoni mwenu ovu, basi na auzuie kwa mikono yake, na ikiwa atashindwa basi auzuie kwa ulimi wake, na akishindwa basi kwa moyo wake.” (Muslim)

مَنْ رَأَى مِنْكُمْ مُنْكَرًا فَلْيُغَيِّرْهُ بِيَدِهِ
فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِلِسَانِهِ فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِقَلْبِهِ
رواه مسلم

MBWA

Kilikuwa ni kipindi cha mavuno na Memis na mkewe walikuwa wanavuna mavuno yao. Pindi walipokuwa akifanya kazi na mtoto wao mdogo alikuwa amelala chini ya mti akitazamwa na mbwa aliyeitwa Karabas.

Muda mfupi baadae Memis na mkewe walipumzika. Walipofika mahala alipolala mtoto wao walishuhudia kitu kibaya. Mtoto wao akiwa amegeuzia uso wake chini, hatikisiki, wakati mbwa Karabas alipokuwa hatua chache tokea eneo hilo, akiwa amerowa damu.

Memis alichanganyikiwa. Alifikiri kuwa karabas amemuua mtoto wake, alimkata mbwa kwa fyekeo. Masikini Karabas alikufa mara moja.

Memis alishituka zaidi wakati mkewe alipomueleza kuwa mtoto wao alikuwa salama, amelala tu. Hawakufikiria chochote hadi walipomuona nyoka mkubwa akiwa amelala mita chache. Waligundua kuwa Karabas alijeruhiwa alipokuwa akipambana na nyoka, na aliyatoa mhanga maisha yake kumuokoa mtoto. Walijiona kuwa wenye makosa makubwa kwa kitendo walichokifanya.

Kama Mamis angefanya kulingana na maamrisho ya Mtume yaliyopo katika hadith ifuatayo wangekuwa ni wenye furaha kubwa:

"Upole unatokana na Allah na haraka inatokana na shetani." (Tirmidh)

الأَنَاةُ مِنْ اللَّهِ وَالْعَجَلَةُ مِنْ الشَّيْطَانِ

رواه الترمذي



NG'OMBE WA MANJANO

Shangazi Aisha alipanda maharagwe katika bustani yake. Maharagwe yalikuwa baada ya muda mfupi kutokana na hali ya hewa kuwa nzuri.

Siku moja Shangazi Aisha Aliamka kutoka na mlio mkubwa wa ng'ombe aliyekuwa bustanini. Alikimbia kuona nini kimetokea. Ng'ombe wa njano wa jirani yake alikata kamba na kuja kwenye bustani yake kuvuruga maharagwe.

Shangazi Aisha alihamanika kuona nguvu zake zinaelekea kupotea bure. Ng'ombe wa njano alikuwa na kamba shingoni mwake, Shangazi Aisha akiwa na hasira alimfuata ng'ombe akiwa na bakora mkononi.

Ni hapo ndipo mke wa jirani yake alipokuja mbio. Alianza kuongea kwa sauti ya huzuni:

"Ndama wake amekufa jana, amekata kamba mara tatu asubuhi hii, anakimbia kimbia kumtafuta mwanae."

Baada ya Shangazi Aisha kusikia hilo fimbo ilimdondoka mkononi, alianza kumchunga ng'ombe huku akimungalia kwa macho ya huruma.

"Kweli…….amemkosa mwanae." alisema.

Hakika alisahau kabisa kuhusiana na maharagwe.

Shangazi Aisha alionyesha huzuni na huruma.

Ni jinsi gani shangazi Aisha alibadilisha muonekano wake, kama alivyoelekeza Mtume wetu mpendwa katika hadith ifuatayo:

"Muogope mungu na usiwe katili kwa wanyama hawa." (Abu Daud)

اتَّقُوا اللَّهَ فِي هَذِهِ الْبَهَائِمِ الْمُعْجَمَةِ

رواه أبو داود

VYANZO VYA Hadith

Ndege: *Nasai*, Kitab al- Imamah, Hadith namba 48.

Mwiba: Tirmidhi, Kitab al – Birr, Hadith namba 16.

Koti: Bukhari, Kitab al- swawm, Hadith namba 56.

Kioo: Abu Dawuud, Kitab al- Adab, Hadith namba 49.

Katili: Bukhari, Kitab al – Madhaalim, hadith namba 3.

Zimwi: Muslim, Kitab al – adhkaar, Hadith namba 38.

Jirani wa peponi: Muslim, Kitab al – adhkaar, Hadith namba 38.

Dawa ya meno: Muslim, Kitab al- Iman, Hadith namba 164.

Pochi: Tirmidhi, Kitab al – Birr, Hadith namba 35.

Sumu: Tirmidhi, Kitab al- Birr, Hadith namba 27.

Mkanda: Tirmidhi, Kitab al- Birr, Hadith namba 58.

Hasira: Bukhari, Kitab al- Adab, hadith namba 76.

Mashindano ya kukimbia: Muslim, Kitab al – Jannah, Hadith namba 64.

Dhahabu: Muslim, Kitab al- Iman, hadith namba 147.

Mwizi: Bukhari, Kitab al- Hudud, Hadith namba 7.

Tonge: Ibn Abi Shaibah, Al- Musannaf (Huut) juz. 6, Hadith namba 164.

Pesa: Muslim, Kitab al- Birr, Hadith namba 5.

Mpatanishi: Tirmidhi, Kitab al – Ilm, Hadith namba 14.

Mchezo wa kutafutana: Tirmidhi, Kitab al- Birr, Hadith namba 37.

Mvurugaji starehe: Tirmidhi, Kitab al- Birr, Hadith namba 58.

Mti wa cheri: Tirmidhi, Kitab al – Zuhd, Hadith namba 27.

Mtoto jasiri: Muslim, Kitab al – 'Itq, Hadith namba 25.

Mtoto wa mbuzi: Ahmad b. Hanbal, Musnad, juz II, Hadith namba 20, 164, 206.

Mtoto mwenye kipaji: Ibn Majah, Kitab al- Adab, Hadith namba 1.

Sahani ya plastiki: Tirmidhi, Kitab al- Birr, Hadith namba 3.

Kalamu: Bukhrai, Kitab al – Adab, Hadith namba 69.

Mwongo: Muslim, Kitab al – Birr, Hadith namba 103.

Mbuyu: Ahmad b. Hanbal, Musnad juz. I, Hadith namba 5.

Mwangwi: Bukhari, Kitab al – Adab, Hadith namba 31.

Mkate: Muslim, Kitab al- Birr, Hadith namba 69.

Bakhili: Tirmidhi, Kitab al –Birr, Hadith namba 40.

Viatu: Ibn Majah, Kitab al- zuhd, Hadith namba 24.

Gari: Muslim, Kitab al – Adab, Hadith, 8.

Moshi: Tirmidhi, Kitab al- Birr, Hadith namba 40.

Matofali: Bukhari, Kitab al- Istqradh, Hadith namba 3.

Mgeni: Tirmidhi, Kitab al- Zuhd, Hadith namba 44.

Mkata kuni: *Abu Dawud, Kitab al- Adab, Hadith namba 44.*

Tupa ya damu: Muslim, Kitab al – Iman, Hadith namba 49.

Mbwa: *Tirmidhi, Kitab al – Birr,Hadith namba 66.*

Ng'ombe wa manjano: *Abu Dawud, kitab al- Jihad, Hadith namba 44.*


TUJIFUNZE
UISLAMU
KIDATO CHA KWANZA
ERKAM


TUJIFUNZE
UISLAMU
KIDATO CHA PILI
ERKAM


ALFABETI ZA
QURAN


MTUME MTEULE
MUHAMMAD
MUSTAFA
1


MTUME MTEULE
MUHAMMAD
MUSTAFA
2

Ustaarabu
wa
Watu wema
AIC


Ustaarabu
wa
Watu wema 2

FOR FREE IN PDF FORMAT

ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT

1350 BOOKS IN **60 LANGUAGES** FOR FREE

Islamic books in different languages are waiting
for you in PDF format at the web site
www.islamicpublishing.org

ERKAM PUBLICATIONS | islamicpublishing.org |